

## Yajue makosa 24 ya rushwa na adhabu inayoweza kutolewa kwa mtu anayepatikana na hatia

Namba	Kifungu	Kosa	Adhabu
1.	15	Kupokea rushwa,kushawishi/kulamzimisha kupewa rushwa,kutoa rushwa au kuahidi kutoa rushwa	Faini isiyopungua shilingi 500,000/=na isiyozidi shilingi 1,000,000/=
			Kifungo kisichopungua miaka mitatu(3)na kisichozidi miaka mitano(5)au faini na kifungo kwa pamoja.
			Pia mahakama yaweza: (i)Kumwamuru mtuhumiwa kumlipa mtu au mwajiri wake kiasi chote au nusu ya pesa au mali aliyopewa rushwa;au (ii)Kutaifisha pesa au mali iliyopokelewa kama rushwa na kuwa mali ya serikali.
2.	16	Kutoa au kupokea rushwa kwa kupata mkataba wa kutoa huduma kwa idara ya umma au shirika la umma	Faini isiyopungua shilingi 3,000,000/= na isiyozidi 3,000,000=
			Kifungo kisichopungua miaka mitatu(3) na kisichozidi miaka mitano au faini na kifungo kwa pamoja
			Pia mahakama yaweza: (i)Kumwamuru kumlipa mtu au mwajiri wake kiasi chote au nusu ya pesa au mali alipewa rushwa;au (ii)Kutaifisha pesa au mali iliyopokelewa kama rushwa na kuwa mali ya serikali.
3.	17	Kutoa au kupokea rushwa ili kumpendelea mtoa rushwa/ kufanikisha kupata tenda katika ununuzi wa mali au huduma katika idara ya serikali,shirika la umma au hata taasisi binafsi.	Faini isiyozidi shilingi 15,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.
			Pia mahakama yaweza: (i)Kumwamuru mtuhumiwa kumlipa mtu au mwajiri wake kiasi chote au nusu ya pesa au mali aliyopewa rushwa;au (ii)Kutaifisha pesa au mali iliyopokelewa kama rushwa na kuwa mali ya serikali.
4.	18	Kutoa au kupokea rushwa ili kutoa upendeleo au kupendelewa katika mnada wowote(unaohusu mali au haki za idara ya serikali,shirika la umma au taasisi binafsi)	Faini isiyozidi shilingi 15,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.
			Pia mahakama yaweza: (i)Kumwamuru mtuhumiwa kumlipa mtu au mwajiri wake kiasi chote au nusu ya pesa au mali aliyopewa rushwa;au (ii) Kutaifisha pesa au mali iliyopokelewa kama rushwa na kuwa mali ya serikali.
5.	20	Kutoa au kupokea rushwa ili kutoa	Faini isiyozidi shilingi 5,000,000/=

		upendeleo au kupendelewa katika suala lolote linalohusu ajira(kuajiriwa au kupandishwa cheo)	Kifungo kisichozidi miaka mitatu (3) au faini na kifungo kwa pamoja
6.	21	Kutoa au kupokea rushwa ili kufanya upendeleo au kumpendea afisa wa shirika la umma kutoka nje ya nchi.	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba (7) Au faini na kifungo kwa pamoja
7.	22	Kutumia nyaraka kwa lengo la kudanganya na kujipatia fedha au faida kwa ufidadi.	Faini isiyozidi shilingi 7,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka miatano(5) au faini na kifungo kwa pamoja.
8.	23	Kujipatia faida au vitu vya aina yoyote kutoka kwa mtu huku mpokeaji wa faida hiyo akijua fika kwamba atatoa maamuzi katika jambo linalomhusu mtoaji wa faida au vitu hivyo.	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba(7) au faini na kifungo kwa pamoja.
			Aidha,mahakama yaweza kuamuru fedha au vitu vilivyopokelewa na mtuhumiwa kutaifiswa na kuwa mali ya serikali.
9.	25	Rushwa ya ngono hutokea pale mtu yeyote aliye na mamlaka au madaraka akiyatumia madaraka hayo kwa kwa kumlazimisha au kumshawishi mtu mwingine kufanya naye tendo la ngono kwa ahadi ya kumpatia ajira,promosheni,au upendeleo fulani.	Faini isiyozidi shilingi 5,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka mitatu (3) au faini na kifungo kwa pamoja.
10.	26(3)	Mtumishi wa umma ambaye amekataa kutoa maelezo au ametoa maelezo ya uongo kwa afisa wa TAKUKURU kuhusiana na mali au akaunti alizonazo anakuwa amefanya kosa la jinai.	Faini isiyozidi shilingi 5,000,000/=Kifungo kisichozidi miaka mitatu(3)au faini na kifungo kwa pamoja.
11	27	Mtumishi wa umma kuwa na mali ambazo mwenye nazo hana maelezo ya kuridhisha kuhusu alivyozipata au kuwa na mali au pesa nyingi kuliko kipato chake halali.	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.
			Mahakama yaweza pia kuamuru mali za mtuhumiwa zitaifishwe na kuwa mali ya serikali.
12	28	Mtumishi wa umma anayefuja mali za umma,au mtumishi katika taasisi binafsi anayefuja mali	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.

		alizokabidhiwa, au anayebadili umiliki na kuwa mali zake	Mahakama pia yaweza kuamuru mali zilizofujwa au kubadilishwa umiliki na mtuhumiwa zirejeshwe kwa mmiliki wake au mtuhumiwa alipe fidia kama mali hizo hazipatikani
13	29	Mtumishi wa umma anayebadilisha matumizi ya mali za serikali au idara ya serikali na kutumika kwa matumizi binafsi.	Faini isiyozidi shilingi 2,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja
14.	30	Mtu yeyote anayemsaidia mtu mwingine kutenda kosa la rushwa kinyume cha sheria hii naye pia anakuwa ametenda kosa la rushwa.	Faini isiyozidi shilingi 2,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja.
15.	31	Mtu anayetumia mamlaka au madaraka aliyopewa na umma kwa manufaa yake binafsi au kwa manufaa ya mtu mwingine.	Faini isiyozidi shilingi 5,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka mitatu (3) au faini na kifungo kwa pamoja.
16.	32	Mtu yeyote anayekula njama na mtu mwingine kwa lengo la kula rushwa kinyume cha sheria hii.	Faini isiyozidi shilingi 5,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka mitatu(3) au faini na kifungo kwa pamoja
17.	33	Mtu yeyote anayefanya ukuwadi wa mamlaka kwa mtu mwenye cheo au madaraka kwa lengo la kumpendelea mtu mwingine na yeye kujipatia faida binafsi (yaani, trading in influence)	Faini isiyozidi shilingi 3,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka miwili(2) au faini na kifungo kwa pamoja.
18.	33	Mtu yeyote anayetumia kuwadi wa mamlaka kumshawishi mtu mwenye cheo au madaraka kwa lengo la kumpendelea ili kujipatia faida binafsi dhidi ya mtu mwingine naye pia anatenda kosa la jinai.	Faini isiyozidi shilingi 3,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au faini na kifungo kwa pamoja.
19	34(1)	Mtu yeyote anayebadilisha au kuhamisha au kuuza mali iliyopatikana kwa njia ya rushwa, au mtu anayeinunua au kukubali kuwa yake mali iliyopatikana kwa njia ya rushwa, anatenda kosa la rushwa.	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/= Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.
20.	4(2),	Mwanasheria Mkuu wa Serikali	Faini isiyozidi shilingi 10,000,000/=

	(3), (4), (5)	anaweza kutoa taarifa/notisi ya maandishi kwa mtu yeyote kumzuia kubadili au kuhamisha au kununua au kukubali kumiliki, mali iliyopatikana kwa njia ya rushwa. Pindi mtu anapopatikana ya kukaidi au kakataa kutekeleza matakwa ya noti hiyo anakuwa ametenda kosa la jinai.	Kifungo kisichozidi miaka saba (7) au faini na kifungo kwa pamoja.
21.	36	Mtu yeyote anayejifanya au anayejitambulisha kuwa afisa wa TAKUKURU, wakati siyo kweli, na anafanya kazi za afisa wa TAKUKURU, anakuwa anatenda kosa la jinai.	Faini isiyozidi shilingi 2,000,000/=
			Kifungo kisichozidi mwaka mmoja(1) au faini na kifungo kwa pamoja
22.	37	Mtu yeyote anayetoa taarifa kwa mtu anayechunguzwa kwa kufanya au kujihusisha na vitendo vya rushwa bila ruhusa ya kufanya hivyo anatenda kosa la jinai chini ya sheria hii.	Faini isiyozidi shilingi 100,000/=
			Kifungo kisichozidi mwaka mmoja(1) au faini na kifungo kwa pamoja.
23	52(3)	Mtu yeyote anayemtishia mtu aliyetoa taarifa za kufanyika au kuwepo kwa mpango wa kufanyika, vitendo vya rushwa anafanya kosa la jinai.	Faini isiyozidi shilingi 500,000/=
			Kifungo kisichozidi mwaka mmoja(1) au faini na kifungo kwa pamoja.
24	3	Afisa yeyote wa TAKUKURU anayemkamata, kumweka kizuizini na hata kumfungulia mashitaka ya uongo mtu yeyote anatenda kosa la jinai.	Faini ya shilingi 1,000,000/=
			Kifungo kisichozidi miezi sita(6) au faini na kifungo kwa pamoja.

Waweza kuwasiliana Na:

TAKUKURU Makao Makuu simu ya Bure: **113**

**Au**

TAKUKURU Mkoa wa Songwe Simu namba: **0744 000 744**

TAKUKURU Wilaya ya Ileje Simu namba: **0744 000748**

**KUMBUKA KUWA:**

**Rushwa Ni Dhambi, Rushwa ni Adui wa Haki na Hudidimiza Taifa. Usishawishi wala usipokee Rushwa.**